

Swahili transcript:

Upendo: Katika hivi vipindi ambavyo kama nilivyosema vimekuwa vikirushwa kwenye televisheni; mara nyingi vimezungumzia sana masuala ya wanawake kujishughulisha. Na mara nyingi utakuta wakina mama labda mbalimbali labda vikundi mbalimbali wanaonyesha vitu ambavyo wanafanya. Kwa mfano, labda ndio hivyo kama usukaji, wengine wanahusika labda na utengenezaji wa maua au kutunza maua nini, wanakuza yale maua baadae wanakuja wanayauza. Mimi nina rafiki yangu, na hiyo mambo haya ya biashara sio kwamba tu mtu kwa vile umekosa kazi ndio ufanye hiyo biashara, unaweza ukawa una kazi yako

Happy: Na bado ukafanya biashara.

Upendo: Na bado ukafanya nini, ukafanya biashara ili nini? kujiongezea kipato. Nina rafiki yangu huyo ambaye ni mwanasheria, lakini pia anajishughulisha na ujasiriamali. Yeye ana hii, hii, ana haya maua. Yeye alinunua miche ya maua, akaitunza nini. Kwa hiyo, siku hizi imeshakuwa mikubwa, ni ile ambayo inatumika kupamba kwenye sherehe za harusi.

Happy: Mmmh?

Upendo: Kwa hiyo sasa hivi, wakati wa harusi ukifika, tayari anapata tenda. Maua yake, ile miti yake nini ndio inachukuliwa inapambwa. Na unajua nini kinatokea? Tena ana Master's, yaani ana ana shahada ya pili katika sheria. Alienda kusoma huko naniii Uholanzi- Nertherlands. Kwa hiyo amerudi, amerudi tu tayari ana master's yake, lakini akawa ameenda pia kujifunza nini-mambo ya upambaji. Sasa ameenda kule katika kujifunza upambaji, anakutana na watu ambao tu wamemaliza tu wengine darasa la saba, wengine labda form four. Yaani wakawa wanamshangaa, huyu vipi? Ana master's bado anakuja huku; lakini walikuwa hawajui mwenzao nini anajifunza. Amejifunza kumbe sio lazima tu ufanye kazi serikalini au mashirika labda ya watu binafsi, lakini pia unaweza ukafanya biashara zako mwenyewe

Happy: Mmmh!

Upendo: Sasa hivi nikiongea nae kwa simu ananiambia huwa anapata tenda kibao yaani. Yaani, anafanya kazi kwenye shirika, haya mambo ya sheria, ana maua yake wakati wa harusi anakodisha, na bado sasa hivi yeye mwenyewe ndiye mpambaji. Kwa hiyo utakuta anapata mpaka laki mbili, laki mbili na nusu katika mpambo mmoja. Kwa hiyo namwambia –rafiki yangu umefika pazuri (kicheko)kwa hiyo wanawake.

Happy: Mwanamke maendeleo

Upendo: Mwanamke maendeleo kwa kweli (kicheko) Okay, vizuri. Na una chochote ambacho unaweza ukazungumzia labda?

Happy: Kwa kweli mimi ningependa kusema tu kwamba wananwake tujishughulishe, tusikae tu nyumbani, tukabweteka, tukategemea hela za kuletewa na wanaume zetu. Hawa wanume wanabadilikaga, tujishughulishe.

Upendo: Tujishughulishe

English Translation:

Upendo: Many television programs in Tanzania recommend that women should occupy themselves with different activities to increase their income. Often television programs show different activities done by women. These include weaving baskets and growing flowers. When the flowers are ready to bloom, flower growers sell them to get some money. It doesn't matter whether you are employed or not to have a business. You can be employed and still have a business to increase your income. I have a friend who is a lawyer by profession, but still she is an entrepreneur. She grows flowers which are used to decorate weddings halls. People rent her flowers for their weddings. As if that is not enough, she has a Master's Degree in Law. She studied in the Netherlands, and when she came back, she took a course in decorating. When she was learning how to decorate, she met people who had only completed elementary or middle school education. They were amazed to see her there because they thought she wouldn't come there because she already had a good education. You can work in government offices or private companies and you still can have a business.

Happy: Yeah!

Upendo: I talk to her frequently on the phone, and she tells me that nowadays she is hired to decorate for weddings and kitchen parties. She gets 200,000 up to 250,000 Tanzanian shillings for one wedding. So women should work hard!

Happy: Women and development...

Upendo: Yeah! Women must succeed! (Laughter) Okay. Do you have anything to add?

Happy: I would advise women to work hard. They should not stay at home and be idle. Women should not depend only on their husbands' income as these men do change. We should also work.

Upendo: Yes, we should work.

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated